

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

14/05/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA AWAPA POLE WAHANGA WA MAFURIKO, ASEMA SERIKALI INAKARABATI MIUNDOMBINU YOTE ILIYOATHIRIWA NA MVUA.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo amefanya ziara ya ukaguzi wa athari za mafuriko ambapo amesema serikali imeanza kukarabati miundombinu iliyoathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha ikiwemo Madaraja, Barabara, Mito na Mifereji.

RC Makonda amesema miongoni mwa maeneo yanayoboreshwa na pesa ipo tayari ni mto msimbazi wenye urefu wa Km 19 na eneo la Jangwani ambalo maboresho yake yatagarimu zaidi ya shilingi Bilioni 200 ikiwa ni mkopo kutoka Bank ya Dunia.

Aidha RC Makonda amesema hadi sasa jumla ya watu wawili wamefariki kutokana na mvua ambapo amewapa pole wananchi waliokumbwa na athari za mafuriko ikiwemo wale ambao mali zao zimeharibiwa na wengine kulazimika kuyaama makazi yao.

Pamoja na hayo RC Makonda amewataka wananchi wanaoishi maeneo hatarishi kuhama huku akiwataka wakazi wa jiji hilo kufanya usafi katika mazingira yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Katika hatua nyingie RC Makonda amewataka wananchi kuchukuwa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Dengue kwa kuhakikisha wanatokomeza mazalia ya mbu na kuhakikisha wanawahi vituo vya afya pindi wanapoona dalili za homa.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM